JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

TAARIFA YA KAMATIYA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KUHUSU UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole,
S.L.P. 941,
41105 **DODOMA.**

Oktoba, 2024

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ..... Error! Bookmark not defined.
SEHEMU YA KWANZA 3
1.0 **UTANGULIZI** 3
1.1 Maelezo ya Jumla 3
1.2 Muundo wa Taarifa 3
1.3 Msingi wa Shughuli za Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma 4
1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 4
1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge 4
1.3.3 Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370 5
1.3.4 Sheria Mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma 5
1.4 Njia zilizotumika 7
1.5 Mambo ya Jumla katika Sehemu ya Utangulizi 7
SEHEMU YA PILI 8
2.0 **UFAFANUZI WA SHUGHULI ZA KAMATIKUFUATILIA MITAJI YA UMMA** 8
2.1 Maelezo ya Jumla 8
2.2 Hali ya Jumla ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma 8
2.3 Tathmini ya Ufanisi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma 9
2.4 Matokeo ya Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma 10
2.4.1 Hali ya Jumla ya makusanyo 10
2.4.2 Kiasi cha Faida Kinachopokelewa na Serikali 13
2.5 Mambo ya Jumla kuhusu uendeshaji wa mitaji ya umma 19
2.5.1 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini 19
2.5.2 Tathimini ya Utendaji wa taasisi na Mashirika ya umma 21
2.5.3 Upungufu wa Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB 26
2.5.4 Baadhi ya Miradi ya Uwekezaji kuanza kabla ya kukamilika kwa maadnalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi 28
2.5.5 Gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji 29
2.5.6 Ujenzi na Uendeshaji wa Stendi ya Msamvu – Morogoro 31
2.5.7 Changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2014 (The VAT Act 2014 [CAP.148 R.E. 2019]) kwenye Kampuni za Madini kwa Soko la Ndani 32
2.5.8 Vigezo vya Utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina 33
2.5.9 Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) 35
2.6 Maoni ya Jumla kuhusu sehemu ya Pili .....**Error! Bookmark not defined.**
SEHEMU YA TATU **..... 38**

3.0 **MAONI NA MAPENDEKEZO** 38
3.1 Maoni 38
3.2 Mapendekezo 39
3.2.1 Uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali 39
3.2.2 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini 40
3.2.3 Tathimini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma 41
3.2.4 Upungufu wa Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB 41
3.2.5 Ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi 42
3.2.6 Wakandarasi wasiokuwa na vigezo kupewa kazi za utekelezaji wa miradi. 43
3.2.7 Gharama za kuunganisha umeme kwa maeneo ya vijiji – miji 43
3.2.8 Uzingatiaji wa vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa hazina. 44
3.2.9 Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) 45
3.2.10 Ujenzi na uendeshaji wa Stendi ya Msamvu 46
SEHEMU YA NNE 47
4.0 HITIMISHO 47
4.1 Shukurani 47
4.2 Hoja 49

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu Uwekezaji wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuliomba Bunge likubali kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inalenga kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya Mwenendo wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali. Nia ni ili kuliwezesha Bunge kujadili na kutoa maazimio yanayoendana na utekelezaji jukumu lake la kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuboresha ustawi wa jamii.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mhesimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu **nne** kama ifuatavyo:-

(a) Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya jumla ambayo ni Utangulizi.

(b) Sehemu ya pili inatoa ufafanuzi wa shughuli za Kamati kuhusu ufuatiliaji wa mitaji ya umma katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

(c) Sehemu ya tatu inabainisha maoni na mapendekezo ili Bunge likiridhia yawe maazimio ya Bunge kwa mambo yaliyojitikeza katika uwekezaji wa mitaji ya umma

(d) Sehemu ya Nne inahitimisha taarifa hii kwa kuliomba Bunge liipokee taarifa na kuijadili.

1.3 Msingi wa Shughuli za Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Msingi wa shughuli zote za Kamatihii, ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (Katiba). Madaraka hayo yanahusu kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote kwa namna iliyowekewa masharti kwenye Kanuni za Bunge. Pamoja na masharti hayo, sheria mbalimbali zilistahili kuzingatiwa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa ufafanuzi zaidi misingi ya shughuli za Kamatini kama ifuatavyo:-

1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi ni hati kuu inayotoa idhini kwa mambo yote ya kisheria, kisiasa na kijamii katika uendeshaji wa shughuli za umma. Kwa maana hiyo, Katiba imekuwa msingi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamatikutokana na kueleza dhamira ya Shughuli zote za umma nchini na kuweka mgawanyo wa madaraka. Aidha, Katiba imekuwa msingi wa shughuli za Kamatihii kwa kuonesha madaraka ya Bunge na kuruhusu kutungwa kwa Kanuni za Bunge zinazoweka utaratibu wa utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Kwa vyovyote vile Kamatihaikupaswa kutoka nje ya msingi huu na kwa kweli masharti yote yalizingatiwa.

1.3.2 Kanuni za Kudumu za Bunge

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinatoa mwongozo kuhusu utaratibu, desturi na uendeshaji wa shughuli zote zinazohusu utekelezaji wa madaraka ya Bunge. Kwa Tanzania, Kanuni za Bunge ni zao la Ibara ya 89 ya Katiba ya Tanzania. Kanuni hizo zimezingatia masharti ya Ibara ya 96 (1) kwa kuanzisha Kamatiza Kudumu za Bunge kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 137 ikisomwa kwa pamoja na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimefafanua majukumu ya Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Majukumu hayo yanahusika na uchambuzi na ufuatiliaji wa uwekezaji wa mitaji ya umma. Ili kutekeleza majukumu hayo, Kamatiilifanya shughuli mbalimbali ikiwemo vikao na ziara. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa, kwa shughuli hizo, Kamatiimefanikiwa kupata undani wa shughuli za uwekezaji wa mitaji ya umma.

1.3.3 Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura ya 370

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), Sura ya 370, imeanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH). Madhumuni ya Kuanzishwa kwake ni utwaaji (*acquisition*), umilikaji (*holding*) na usimamizi (*management*) wa mitaji ya umma kwa niaba ya Serikali. Kwa mujibu wa Sheria hii, mitaji ya umma ni pamoja na hisa (shares), hati fungani (government bonds), dhamana ya hisa ya mikopo, rehani ya ndani au nje ya bodi inayotambulika kisheria, ambayo imetolewa na Serikali au kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu na madaraka ya Msajili wa Hazina (TR) katika uwekezaji wa mitaji ya umma unaofuatiliwa na Kamatiyamebainishwa katika Sheria hii. Kwa msingi huo, Kamatiilipofuatilia mitaji ya umma ilitathmini uendeshaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo kuna ukubalifu (*Compliance*) wa masharti ya Sheria hii kuhusu usimamizi wa mitaji ya umma.

1.3.4 Sheria Mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), sheria nyingine zinazofafanua masharti kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma zilizingatiwa wakati wa kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma. Sheria hizo kutaja baadhi, ni Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya

257, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 na Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mashirika ya Umma imeweka masharti kuhusu uanzishaji, usimamizi, uongezaji wa ufanisi na mambo mengine yanayohusiana au yanayowezesha madhumuni hayo. Kwa msingi huo, Kamati, ilizingatia masharti ya Sheria hii na kutathmini iwapo uwekezaji na usimamizi wa mitaji katika mashirika ya umma unafanyika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha za Umma, imeweka masharti ya udhibiti (*contral*), usimamizi (*Management*) na urekebu (*Regulation*) wa makusanyo na matumizi ya fedha za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, sheria hii imebainisha masharti ya udhibiti na usimamizi wa kibunge wa fedha na rasilimali za umma. Vilevile sheria inatambua kwamba, fedha zinazotumika katika mtaji wa umma, mali zilizopo katika vitega uchumi vitokanavyo na fedha za umma na mikopo katika uendeshaji wa vitega uchumi ni sehemu ya rasilimali za umma. Kamatiilitathmini chumo (*returns*) kutokana na fedha za umma linapaswa kuangaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, inampa Msajili wa Hazina Madaraka na Majukumu ya kusimamia fedha zinazotolewa kwa ajili ya uwekezaji kwenye taasisi au mashirika anayoyasimamia. Kwa mujibu wa sheria hiyo, Msajili wa Hazina analo jukumu na madaraka ya kuhakikisha kwamba mashirika na taasisi anazozisimamia zinalipa magawio na michango stahiki kwa Serikali. Kamatiilifuatilia kujua utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili ya kusimamia fedha zinazotumika katika mitaji ya umma.

1.4 Njia zilizotumika

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, naomba kubainisha mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamatikwa kipindi kinachoripotiwa. Mbinu hizo ni:-

(i) Kuchambua masharti ya Sheria inayohusika na uwekezaji uliofanyika kwa lengo la kubaini uhalali wake na uendeshaji uliotakiwa;

(ii) Kupokea na kuchambua Taarifa za Msajili wa Hazina (TR) kuhusu hali ya jumla ya mitaji ya umma kwenye taasisi na mashirika ya umma au kwenye Kampuni ambapo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma;

(iii) Kufanya mahojiano na menejimenti na Bodi za taasisi au mashirika ambayo yanatumia mitaji ya umma. Lengo ni kuthibitisha usahihi wa hali ya mitaji ya umma kwenye taasisi husika kabla ya kutoa taarifa Bungeni; na

(iv) Kutembelea na kukagua hali ilivyo kwenye baadhi ya miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na taasisi na mashirika ambayo yanatumia mitaji ya umma.

1.5 Mambo ya Jumla katika Sehemu ya Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Jumla ya yote katika sehemu hii, Taarifa inatambulisha maudhui, madhumuni na misingi ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati. Kwa ujumla, Taarifa hii inahusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Madhumuni yake ni kulijulisha Bunge hali ilivyo sambamba na kushauri hatua stahiki. Kadhalika, Taarifa hii inatokana na misingi ya masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na Sheria mbalimbali zinazohusu uwekezaji wa mitaji ya umma.

SEHEMU YA PILI

2.0 UFAFANUZI WA SHUGHULI ZA KAMATI KUFUATILIA MITAJI YA UMMA

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inatokana na ukweli kwamba, uwekezaji wa mitaji ya umma ni nyenzo muhimu inayotumiwa na Serikali katika kukuza uchumi na kupata faida. Sambamba na hilo, mafanikio ya uwekezaji yanategemea uzingatiaji wa mambo ya muhimu kama vile misingi ya utawala bora katika vitegauchumi pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa uwekezaji. Kwenye mambo hayo, Bunge limepewa nafasi muhimu ya usimamizi wa shughuli za umma ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Ili Bunge lichukue nafasi yake ya usimamizi unaostahili, Kamatiya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, hufuatilia mwenendo na masuala mengine ya mitaji ya umma kwa lengo la kutoa taarifa na mapendekezo kwa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo niliioueleza, sehemu hii inaripoti shughuli zilizofanyika katika kufuatilia ufanisi wa uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, uchambuzi wa hali iliyobainika unaripotiwa ili kuliwezesha Bunge kuamua kulingana na madaraka yake.

2.2 Hali ya Jumla ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, uwekezaji wa mitaji ya umma ni aina ya uwekezaji ambapo Serikali, kwa niaba ya wananchi, inatumia fedha za umma ili kuwekeza katika miradi mbalimbali ya vitegauchumi au mitaji ya kampuni. Mitaji inaweza kuwa katika namna ya hisa, dhamana au aina nyingine za ushiriki kwenye umiliki. Malengo ya uwekezaji huu ni pamoja na kukuza uchumi kwa kuwekeza katika kampuni zinazofanya vizuri ili kusaidia

kuongeza ajira, kuchochea biashara na kuimarisha ukuaji wa uchumi na kupata faida ambayo ni sehemu ya chumo la uwekezaji. Lengo lingine ni kusaidia sekta za kipaumbele kama vile sekta za teknolojia, nishati mbadala au kilimo ili kuchagiza ukuaji wa sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya jumla ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inaonesha kuwa thamani ya mitaji ya umma katika mashirika, taasisi za umma na kampuni mbalimbali ni **shilingi trilioni 75.79**. Uwekezaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 3 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **trilioni 73.36** kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kiasi hicho cha mtaji kimewekezwa kwenye maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza ni taasisi ambapo Serikali ina hisa asilimia 51 au zaidi na la pili ni taasisi au kampuni ambapo Serikali ina hisa chache (asilimia 50 au pungufu).

Mheshimiwa Spika, Taarifa zilizochambuliwa zinaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, Serikali ilikuwa imewekeza jumla ya **Shilingi trilioni 2.82** katika kampuni ambapo kiasi cha Shilingi **trilioni 2.04** kilikuwa kimewekezwa katika Kampuni ambazo zinaendesha shughuli zake ndani ya nchi na **Shilingi bilioni 778.95** katika Kampuni ambazo zipo nje ya nchi.

2.3 Tathmini ya Ufanisi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kufanya kazi kwa misingi na viwango, tathmini ya ufanisi ilifanyika kwa kuzingatia vigezo maalum wakati wa kufuatilia uwekezaji. Vigezo hivyo vinaendana na masharti ya Kanuni ya 11 (1) na (2) ya Kanuni za Bunge. Jambo moja la msingi lilihusu kuangalia mambo ya ujumla yanayopima ufanisi wa mitaji ya umma kwenye taasisi, mashirika ya umma na kampuni ambapo Serikali ina umiliki wa hisa. Orodha ya mambo hayo ya ujumla ni kama ifuatavyo:-

(a) Kiasi cha faida kinachopokelewa na Serikali kutokana na hisa zake kwenye vitegauchumi mbalimbali ambacho ni gawio (dividend);

(b) Kiasi cha mchango utokanao na 15% ya mapato ghafi kutoka Taasisi na Mashirika ya umma yanayostahili kuchangia kwa mujibu wa Sheria (*Contribution to the Consolidated Fund*);

(c) Kiasi cha michango kutokana na makusanyo ya ziada na michango mingine (*Surplus and other remittances*); na

(d) Vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo ni viashiria vinavyosaidia kubaini, iwapo uwekezaji wa mitaji ya umma unafanyika kwa ufanisi na kuwa umezingatia miongozo mujarabu. Aidha, uchanganuzi wa kina wa vigezo hivyo, unasaidia kubaini kiwango cha uzingatiaji wa miongozo na misingi ya biashara. Naomba kulihakikishia Bunge kwamba, mambo hayo yaliongoza uchambuzi na tathmini iliyofanyika ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

2.4 Matokeo ya Ufuatiliaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, lina madaraka ya kusimamia shughuli za umma ikiwemo uwekezaji wa mitaji ya umma. Kwa utaratibu wake, Bunge linatumia Kamatiya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kufuatilia mwenendo wa mitaji ya umma. Hivyo, Kamati inaripoti matokeo ya ufuatiliaji ili kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi wa kibunge. Kwa msingi huo, Taarifa hii inatoa matokeo ya ufauatiliaji kama ifuatavyo:-

2.4.1 Hali ya Jumla ya makusanyo

Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali kutokana na uwekezaji wa mitaji ya umma kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni shilingi **trilioni 1.008**. Kiasi

hiki ni jumla ya mapato kutokana na mtaji kwenye taasisi ambazo Serikali ina hisa kubwa na ambao Serikali ina hisa chache. Mchanganuo wa aina hizo za mapato ulifanyika ili kutathmini ufanisi wa kila aina ya uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kipindi hicho. Taswira ya hali hiyo inaonekana katika Jedwali Na. 01 la Taarifa hii.

MAPATO YASIYO YA KODI	KIASI KILICHOLIPWA		TOFAUTI KATIKA %
	2021/2022	2022/2023	
Gawio	357,528,737,004.51	328,746,772,163.71	-8%
Michango (15%)	324,025,703,627.12	346,280,991,227.57	7%
Ziada & Michango Mengineyo	105,017,840,361.84	287,212,061,547.52	173%
Riba na Marejesho ya Mikopo	54,227,849,370.00	36,039,502,125.00	-34%
Wasilisho la TTMS	9,481,254,946.67	10,109,407,646.50	7%
	850,281,385,310.14	**1,008,388,734,710.30**	**19%**

Chanzo: **Majumuisho ya Kamati kutokana na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa na Msajili wa Hazina**

Mheshimiwa Spika, hali ya jumla inayoonekana katika Jedwali hilo inaarifu mambo mablimbali yanayoweza kufafanuliwa kwa kutumia grafu Na. 01 na Na. 02 zifuatazo:-





Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kama ifuatavyo:

(i) Kwa ujumla mapato yasiyo ya kikodi kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 19 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Katika ongezeko hilo ziada na michango mingineyo ambayo imeongezeka kwa kiwango cha asilia 173.

(ii) Kiasi cha michango iliyopokelewa kutokana na asilimia 15 ya mapato ghafi ya taasisis zilizostahili kuchangia pamoja na wasilisho la TTMS, kila kimoja kiliongezeka kwa asilima 7;

(iii) Mapato ya gawio kwa mwaka 2022/2023 yamepungua kwa asilimia asilimia 8, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, gawio lilichukua sehemu kubwa ya mapato yasiyo ya kikodi kwa kufikia asilimia 42. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 mchango wa gawio katika mapato ulipungua kufikia asilimia 33 ya mapato yasiyoya kikodi yaliyokusanywa.

(iv) Mwaka wa fedha 2021/2022 ziada na michango mingineyo ilichangia mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mitaji ya umma

kwa asilimia 12 tu. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 mchango wake uliongezeka na kufikia 34 ya mapato yasiyo ya kikodi kutokana na mtaji wa umma.

2.4.2 Kiasi cha Faida Kinachopokelewa na Serikali

Mheshimiwa Spika, kila mwekezaji anayewekeza kwa kumiliki hisa hutarajia kupata faida inayotokana na mtaji uliowekezwa. Serikali inapotumia mtaji wa umma na kumiliki hisa inapaswa kupata kiasi cha faida kinachostahili. Ili kubaini ufanisi wa mtaji wa umma unaotumika kwenye umiliki wa hisa, tathmini ya kiasi cha faida kinachopokelewa na Serikali kwa namna ya gawio ni muhimu kwa Kamati. Ili kutathmini ipasavyo, Kamati iliainisha uwekezaji wa Serikali katika taasisi ambako ina hisa chache na uwekezaji katika taasisi ambako ina hisa nyingi kama ifuatavyo:-

(a) Uwekezaji kwenye taasisi ambako Serikali ina hisa chache

Mheshimiwa Spika, Taarifa za uwekezaji zilionesha kuwa thamani ya hisa za Serikali katika taasisi ambapo Serikali ina hisa chache ilitofautiana kwa miaka miwili. Aidha, idadi ya kampuni au taasisi ilitofautiana kwa mwaka 2022/2023 na 2021/2022. Wakati kwa mwaka 2022/2023 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 50, mwaka 2022/2023 Serikali ilikuwa na hisa chache kwenye taasisi 56 Ongezeko hilo la taasisi ni asilimia 12.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kiasi cha gawio kilichopokewa na Serikali ulionesha kuwa kuna tofauti kati ya mwaka 2022/2023 na mwaka 2021/2022. Kwa mwaka 2022/2023, Serikali ilipokea gawio la kiasi cha shilingi Bilioni 231.2 kutoka taasisi 15 kati ya 56 na mwaka 2021/2022 Serikali ilipokea kiasi

cha Shilingi Bilioni 204.37 kutoka taasisi 14 kati ya 50. Mchanganuo bayana unaonekana katika Jedwali Na. 01.

Jedwali Na. 1 Mchanganuo wa Hisa na Gawio kwenye Taasisi au Kampuni ambako SAerikali ina hisa chache

MWAKA	IDADI YA TAASISI ZILIPO HISA CHACHE	(TRILIONI) THAMANI YA HISA CHACHE	KIASI CHA GAWIO
2021/2022	50	2.56	204.37
2022/2023	56	2.56	231.2
TOFAUTI YA KIASI	6	0.24	26.83
ASILIMIA	12	9	13

Chanzo: Majumuisho ya PIC

Mheshimiwa Spika, Jedwali hilo linaonesha kama ifuatavyo:-

(i) Idadi ya Taasisi ambapo Serikali ina hisa chache iliongezeka kwa asilimia 12 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023;

(ii) Thamani ya hisa za Serikali kwenye Taasisi au Kampuni ambapo Serikali ina hisa chache iliongezeka kwa asilimia 9 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022; na

(iii) Kiasi cha gawio kilichopokelewa na Serikali kwa mwaka 2022/2023 kiliongezeka kwa asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinatoa maelezo ya ufanisi wa mtaji wa umma kwa namna tofauti. Kwanza, inaonesha kuwa juhudi za Serikali kuwekeza katika kampuni zinazolipa faida zinaongezeka. Ushahidi wa hili ni ongezeko la idadi ya taasisi ambapo Serikali inawekeza na ongezeko la thamani ya hisa za Serikali ikilinganishwa na mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la ufanisi wa mtaji wa Umma linaonekana kwenye ulinganisho kati ya ongezeko la thamani ya hisa na ongezeko la kiasi cha gawio. Wakati thamani ya hisa imeongezeka

kwa asilimia 9, kiasi cha gawio kimeongezeka kwa asilimia 13. Kwa maneno mengine ongezeko dogo kwenye thamani ya hisa limesababisha ongeko kubwa la gawio.

(b) Uwekezaji kwenye taasisi na Mashirika ambako Serikali ina hisa nyingi

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa mtaji wa umma kwenye mashirika, kampuni au taasisi ambapo Serikali ina hisa nyingi unaweza kupimwa kwa kuangalia mapato yasiyo ya kikodi yanayojumuisha gawio, michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi na ziada na michango mingineyo yanayokusanywa kutoka kwenye taasisi hizo. Upimaji huo unafanyika kwa kulinganisha mchango wa taasisi hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa miaka miwili tofauti ya uwekezaji. Kwa urahisi wa ufafanuzi, Jedwali Na. 03 linaonesha taswira ya ufanisi.

Jedwali Na. 3 Uwekezaji kwenye taasisi na Mashirika ambako Serikali ina hisa nyingi na mchango kutoka kwa taasisi hizo

MWAKA WA FEDHA		IDADI YA TAASISI AMBAKO KUNA HISA	THAMANI YA HISA	KIASI CHA MAPATO YASIYO YA KIKODI
2021/2022		248	70.8	699.9
2022/2023		250	72.97	789.4
TOFAUTI		2	2.17	89.5
ASILIMIA		0.8	3.1	11.3

Mheshimiwa Spika, Jedwali hili linaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Serikali imeongeza idadi ya Mashirika, Kampuni na Taasisi ambako ina hisa nyingi kutoka 248 mwaka 2021/2022 hadi 250 mwaka 2022/2023;

(ii) Thamani ya hisa kwenye maeneo ya uwekezaji ambapo Serikali ina hisa nyingi imeongezeka kutoka shilingi trioni 70.8 mwaka 2021/2021 hadi shilingi trilioni 72.97 mwaka 2022/2023.

(iii) Ongezeko la maeneo ya uwekezaji wa mitaji ya umma halitofautiani sana na ongezeko la thamani ya hisa za Serikali.

i) Gawio

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/23 kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika mashirika ya umma ambayo Serikali inaumiliki wa hisa nyingi kilikuwa jumla ya **shilingi bilioni 109**, kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 47.4 ulilinganisha na kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika taasisi hizi kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambapo gawio lilikuwa **shilingi bilioni 207.2**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kiasi cha gawio kilichokusanywa kutoka katika mashirika yanayojiendesha kibiashara kilichangiwa na mashirika 9 kati ya 33 yanayopaswa kuchangia, sawa na asilimia 27.3 ya Mashirika yaliyotoa gawio kupitia kipengele hiki. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iimarishe mikakati ya kuyasimamia mashirika haya ili kuhakikisha ya najiendesha kwa ufanisi na kupata faida ili yaweze kutoa gawio. Aidha, Serikali iweke mifumo ya uwajibishaji kwa ambao hawatekelezi agizo hili la kisheria.

ii) Michango ya Asilimia 15 ya Mapato ghafi

Mheshimiwa Spika, Michango ya Asilimia 15 ya mapato ghafi ineonesha ufanisi wa mitaji ya umma kwenye taasisi stahiki. Kwa mwaka 2020/2021 makusanyo yalikuwa ni Sh. Bilioni 202.2, mwaka 2021/2022 yalikuwa shilingi Bilioni 324 na mwaka

2022/2023 yalikuwa ni shilingi Bilioni 346.3. Mwenendo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Na. 04

Jedwali Na. 4 Mchango wa asilimia 15 katika Mfuko Mkuu wa Serikali

MWAKA	KIASI KILICHOKUSANYWA(BILIONI)	ONGEZEKO AU PUNGUZO (BILIONI)	%
2020/2021	**202.2**	**-**	**-**
2021/2022	**324**	**121.8**	**37.5**
2022/2023	**346.3**	**22.3**	**6.4**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo:

(i) Mwaka 2021/2022 kiasi cha michango ya Asilimia 15 kiliongezeka kwa asilimia 37.5 ambacho ni kiasi kikubwa.

(ii) Mwaka 2022/20-23 kiasi cha michango ya Asilimia 15 ya mapato ghafi iliongezeka kwa kiasi cha 6.4 tu.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa, ufanisi wa ukusanyaji wa michango ya 15% ya mapato ghafi umekuwa ukiongezeka ambapo kwa mwaka 2021/22 uliongezeka zaidi kwa asilimia 37.5 na mwaka 2022/2023 uliongezeka kwa asilimia 6.4 tu. Hivyo, kwa ujumla wake ufanisi umeongezeka. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini pia, pamoja na ufanisi wa michango hii kuongezeka mwaka 2022/23 lakini idadi ya taasisi zilizochangia zilipungua kutoka taasisi 25 mwaka 2021/22 hadi taasisi 23 mwaka 2022/23 kati ya taasisi 28 zinazopaswa kuchangia chini ya kipengele hiki. Kwa maneno mengine ni kwamba kipengele hiki bado hatujakitumia kwa ukikamilifu, kama kitasimamiwa kiakamilifu na taasisi na mashirika

yote yakachangia kwa mujibu wa sheria, Serikali itapata mapato mengi zaidi kupitia kifungu hiki.

iii) Ziada na Michango mingineyo

Mheshimiwa Spika, kipengele cha ziada na michango mingeyo kinajumuisha asilimia 70 ya ziada ya mapato inayotokana na shughuli kwa taasisi zinazotoa huduma na michango ya hiyari na mapato yanayotokana na shughuli za ufuatiliani zinazofanywa na Msajili wa Hazina. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 kipengele hiki kimekuwa na ufanisi ambapo jumla ya shilingi 287.2 zilikusanywa kiasi ambachi ni ongezeko la aslimia 63.4 ukilinganisha na kiasi cha shilingi 105 kilichokusanywa mwaka 2021/22.

Jedwali Na. 5 Michango ya Ziada na michango mingeyo

MWAKA	TAASISI	KIASI (BILIONI)
2021/2022	**107**	**105**
2022/2023	**85**	**287**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamatiumabaini mambo yafuatayo:-

(i) Mwaka 2021/2022 kiasi cha michango ya ziada na michango mingineyo kiliongezeka kwa asilimia 63.4 ambacho ni kiasi kikubwa.

(ii) Idadi ya taasisi zilizochangia kwa kwaka 2022/23 zimepungua kwa asilimia 25.8 ingawa mchango umeongezeka.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba taasisi na mashirika ya umma yakisimamiwa kikamilifu na kuongeza ufanisi wake yanaweza kuongeza mchango wake katika mfuko wa Serikali na tija hasa ya uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali ikaweza kupatikana.

2.5 Mambo ya Jumla kuhusu uendeshaji wa mitaji ya umma

Mheshimiwa Spika, Kifungu 11(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Februari, 2023 kinaipa Kamati jukumu la kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa. Katika kutekeleza jukumu hilo Kamati ilibaini mambo mbalimbali ya kiutendaji ambayo ni pamoja na;-

2.5.1 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini

Mheshimiwa Spika, taasisi na mashirika ya Umma yameendelea kuwa chachu ya ukuaji wa Uchumi katika nyanja mbalimbali ikiwemo uzalishaji, usafirishaji, mawasiliano, elimu, udhibiti, utalii, maji, miundombinu na huduma za kifedha. Aidha, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji ili kuhakikisha huduma stahiki zinatolewa kwa wanachi na vilevile mashirika yanajiendesha kwa faida kufanya uwekezaji zaidi na kuweza kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, moja ya kigezo cha utendaji ambacho taasisi na mashirika ya umma wamewekewa na Msajili wa Hazina ni kuhakikisha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini unapungua mwaka hadi mwaka lakini kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma hayajafanikiwa kutekeleza kigezo hiki na badala yake yamekuwa yakiongeza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utendaji wa Msajili wa hazina kwa Mwaka wa fedha 2022/2023 utegemezi wa Ruzuku umeongezeka ambapo kwa miaka mitatu mfululizo umekua kwa asilimia 21.2 kutoka **shilingi bilioni 13.234 m**waka 2021/2022 hadi kufikia **shilingi Bilioni 17.456** mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ilibaini kuwa kuna mashirika Sitini na Tatu (63) ambayo kutokana na uendeshaji wa shughuli zake yanapata mapato makubwa kuliko ruzuku wanayopokea kutoka Serikali

lakini bado yanapokea Ruzuku kutoka Serikali. Ni vema Mashirika haya yakasimamiwa kikamilifu kuhakikisha yanatekeleza majukumu yake kikamilifu, yanakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji mapato na yanadhibiti matumizi yake kisha yakapewa mpango wa kujiondoa kwenye utegemezi wa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini pia katika ya mashirika Thelethini na Tano (35) yanayojiendesha kibiashara, mashirika Kumi na Saba (17) yanapokea ruzuku kutoka Serikalini. Mashirika haya yanapaswa kuongeza ufanisi, kutumia fursa zilizopo sokoni ili kuongez mapato yake na hatimaye kujitoa katika utegemezi wa ruzuku.

Aidha, Kabati ilibaini utegemezi wa Ruzuku ya matumizi mengineyo pamoja na mishahara umeongezeka pia, ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2022/23 imeeleza kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo utegemezi wa matumizi mengineyo na mishahara umeongezeka kutoka shilingi bilioni 793.58 mwaka 2021/222 hadi shilingi trilioni 1.33 Mwaka 2022/23, ongezeko hili ni sawa na asilimia 40.64 ambao ni ongezeko kubwa.

Mheshimiwa Spika, mategemeo ya Serikali kuanzisha taasisi na mashirika ya umma ni pamoja na yajiendeshe kwa ufanisi, yatoe huduma stahiki kwa wadau wake yaweze kutengeneza faida na hatimaye kuweza kujitegeme katika uendeshaji wake kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iyasimamie kikamilifu na kuyawekea mpango muda mfupi na wakati wa kujitoa kwenye utegemezi wa ruzuku ili kuipunguzia Serikali mzigo.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuyawezesha mashirika kujikitegemea na kujitoa katika utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini, Ofisi ya Msajili wa Hazina inahitajika kuongeza juhudi katika kufanyiwa

marekebisho/maboresho katika taasisi husika. Maboresho haya yahusishe kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na mifumo ya ukusanyaji wa mapato; na kurekebisha gharama za uendeshaji ili kuhakikisha mapato, matumizi na ufanisi wa taasisi vinaendana; na kuboresha mbinu na mikakati ya biashara kwa mashirika yanayojiendesha kibiashara ili yaweze kushindana katika soko na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

2.5.2 Tathimini ya Utendaji wa taasisi na Mashirika ya umma

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370, Kifungu cha 7 (1) imepewa Msajili wa Hazina jukumu la kusimamia uwekezaji na mali nyingine za Serikali katika taasisi, mashirika, wakala za Serikali na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa au kuna maslahi ya umma kwa niaba ya Mhe. Rais na kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha mitaji katika taasisi, mashirika na taasisi za umma inasimamiwa ili kuleta tija, Kamati ilipitia taarifa za utendaji wa baadhi ya taasisi ili kujiridhisha kuhusu utendaji wake. Uchambuzi uliofanyika kwenye eneo hilo ilikuwa kuangalia vyanzo vya mapato; mwenendo wa mapato yanayopatikana kama yanatosha kuendesha shughuli mbalimbali za taasisi hizo; matumizi ikilinganishwa na ukomo wa bajeti; ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za taasisi; madeni ya taasisi na mwenendo wa ulipaji; na faida inayopatikana kutokana na utendaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika na wakala za Serikali utendaji wake unasuasua, jambo ambalo linaathiri tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma. Mambo yaliyobainika katika uchambuzi wa Kamatini pamoja na:-

i) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamepata hasara au nakisi kwa miaka mitatu mfululizo

Uchambuzi unaonesha kuwa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamepata hasara /nakisi katika kipindi cha miaka miwili mfululizo. Hali hii inatokana na Bodi na menejimenti za taasisi hizo kuwa na usimamizi usioridhisha na hivyo kusababisha kukosekana kwa ufanisi, ikiwemo kutokuwa na ubunifu katika kuendeleza vyanzo vilivyopo vya mapato na vilevile kushindwa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha utendaji wa taasisi unakuwa na tija. Mfano wa taasisi hizo ni pamoja na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Maendelo ya Petroli (TPDC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Bodi ya Mkonge (TSB), Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC), Mamlaka ya Elimu ya Juu n.k Hali ya kupata hasara mfululizo inaleta mashaka katika uendelevu wa taasisi na inaweza kusababisha malengo ya uanzishwaji wa taasisi hizi kutofikiwa. Hivyo, kuna umuhimu wa utendaji wa taasisi hizi ukatathiminiwa upya kwa lengo la kuboresha utendaji ili kuleta tija ya uwekezaji.

ii) Hali mbaya ya Ukwasi kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya Umma.

Ukwasi wa mashirika ya umma ni uwezo wa shirika la umma kutimiza wajibu wake wa kifedha kwa wakati na kwa kiasi kinachohitajika. Kwa maneno mengine, ni uwezo wa shirika la umma kulipa madeni yake ya muda mfupi na kubaki na fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za shirika.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kutokuwa na ukwasi wa kutosha hali

ambayo umesababisha mashirika mengi kujiendesha kwa madeni kutokana na kutumia huduma za wazabuni bila kulipia. Mfano wa mashirika ya umma ambayo kwa miaka mitatu mfululizo yamekuwa yakizalisha madeni ni pamoja na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bodi ya Mkonge Tanzania n.k.

iii) Baadhi ya taasisi na Mashirika ya umma kuwa na Mitaji mikubwa isiyozalisha (non – productive assets)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi pia umebainisha kwamba kuna baadhi ya mashirika yana mitaji mikubwa ambayo haizalishi (non-productive assets). Mitaji hiyo ni kama vile majengo, ardhi, mitambo iliyopitwa na wakati ambayo haina ufanisi ikilinganishwa na teknolojia iliyopo kwa sasa katika uzalishaji. Hesabu za mashirika husika zinaonyesha kiwango kikubwa cha mtaji lakini ukiangalia uwezo wa mtaji huo kuzalisha unakuwa mdogo hivyo kutoa tija ndogo ya uwekezaji. Mfano wa mashirika yaliyo na changamoto hiyo ni pamoja na TTCL, NIC, NDC na TPC. Hivyo, ni muhimu kufanyika kwa uchambuzi wa kina ili kuangalia uwezekano wa mashirika haya kubaki na mali ambazo zinazalisha ili kuepusha kuwa na mali nyingi ambazo zinaongeza gharama za uendeshaji.

iv) Baadhi ya taasisi na Mashirika ya umma kushindwa kutumia fursa walizo nazo

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi pia umebainisha kwamba, baadhi ya mashirika ya umma pamoja na uwepo wa ushindani na sekta binafsi bado yana fursa kwenye ushindani kutokana na majukumu yao lakini hayajaweza kutumia fursa hizo kikamilifu. Mashirika hayo

ni pamoja na TTCL kwenye soko la mawasiliano ambapo kuna fursa kupitia mradi wake mkubwa wa fibre mlangoni. Aidha, ranchi ya NARCO ina nafasi ya kushindana kwenye soko la uzalishaji wa mifugo na mazao yake; CPB kwenye soko la nafaka; na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) kwenye masuala ya uvuvi kibiashara. Mashirika haya ni yale yanayojiendesha kibiashara, ni vema Serikali ikatathimini uendeshaji wa mashirika haya na kuyawezesha kwa maeneo ambayo ni kikwazo kwayo ili yaweze kujiendesha kiukamilifu na kuweza kushindana katika soko na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

v) Baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yana Upungufu wa mtaji wa uendeshaji

Mheshimiwa Spika, uchambazi wa Kamati ulibaini kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mtaji wa uendeshaji jambo linaloathiri utendaji wa shirika husika. Changamoto hii imepelekea baadhi ya taasisi na mashirika ya umma kujiendesha kwa kutumia mtaji kidogo au hasi kabisa jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi, mfano wa taasisi hizo ni pamoja na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Boharii ya Dawa (MSD), Benki ya Maendeleo (TIB DFI).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mapato ya Serikali ukilinganisha na mahitaji ya fedha ni vema taasisi na Mashirika ya umma yaliyo na fursa za kuwekezaji yaelekezwe kutumia njia mbadala za upatikanaji wa fedha kama vile PPP, Mikopo kutoka taasisi za fedha, na vilevile kutumia fursa ya upatikanaji wa fedha kupitia soko la hisa ambapo mashirika yanaweza kuuza hisa au kuuza hati fungani (bond) kwenye soko kwa lengo la kupata mitaji ya

utekelezaji wa shughuli zao na hatimaye kuweza kupunguza utegemezi wa Ruzuku.

vi) Upatikanaji wa vibali vya ajira na mchakato wa kuajiri

Mheshimiwa Spika, ili mashirika ya biashara yaweze kujiendesha kwa ufanisi yanatakiwa kuwa na watumishi wenye uwezo wa kushindana kwenye soko na kampuni katika sekta binafsi. Uchambuzi umebaini baadhi ya mashirika yanayojiendesha kibiashara yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi kutokana na kuchelewa kwa vibali vya ajira kutoka kwenye za Serikali. Mfano wa mashirika yaliyokumbwa na changamoto hii ni pamoja na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) ambayo imepewa kibali cha kutoa ajira za ukomo wa miaka miwili jambo ambalo linasababisha Bodi kupoteza wafanyakazi wengi ambao tayari iwamejengea utaalamu wa kutosha kupitia fedha za shirika. Hivyo, kutokana na masharti hayo kila baada ya miaka miwili Bodi hiyo hutakiwa kuajiri watumishi wengine na kuanza kuwajengea tena uwezo hali ambayo kwa upande mwingine inadhorotesha utendaji kazi na vilevile kuongeza gharama kwa shirika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuwezesha taasisi na mashirika ya umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Juhudi hizo zinazofanywa na Serikali, zitaonekana kuwa na tija endapo mashirika haya yatajiendesha kwa ufanisi, kutoa huduma stahiki na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha tija katika uendeshaji wa mashirika ya biashara, Kamati ilikuwa na maoni kwamba yapatiwe uhuru wa uendeshaji ikiwemo uhuru wa kuajiri ili yaweze

kujiendesha kwa ushindaji na hivyo tija ya uwekezaji iweze kupatikana. Aidha, kwa taasisi ambazo hazifanyi biashara bali zinatoa huduma kwa jamii zisimamiwe ili kuhakikisha zinatekeleza wajibu wake kikamilifu kwa lengo la kutoa huduma stahiki kwa ustawi wa jamii yetu.

2.5.3 Upungufu wa Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo (TIB) ni taasisi ya maendeleo ya fedha (development finance institution) iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki ya Rasilimali Tanzania iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 6 Novemba, 1970. Benki hii imeanzishwa kwa lengo kubwa moja ambalo ni kutoa huduma za fedha kwa miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu ili kujenga taifa lenye uchumi shirikishi, mseto na wenye ushindani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya uwekezaji wa Benki ya Maendeleo TIB na kubaini kuwa uendeshaji wa benki hii sio wa kuridhisha. Mambo yaliyobainika katika utendaji wa benki hii ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya TIB ilipata hasara kabla ya kodi, mwaka 2023 hasara ilifikia shilingi bilioni 5.92 ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo hasara kabla ya kodi ilikuwa shilingi bilioni 131.97. Hasara hii ilichangiwa zaidi na kufutwa kwa mikopo chechefu iliyorithiwa kutoka iliyokuwa Benki ya TIB Corporate. Aidha, hasara iliyopatikana ilisababisha Rejesho la mtaji kuendelea kushuka kutoka asilimia 2.7 mwaka 2022 hadi rejesho hasi mwaka 2023. Benki inahimizwa kuongeza ufanisi katika uendeshaji wake ili kuzalisha faida ili kukuza rejesho la mtaji kuendana na ukomo uliowekwa wa asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa mwongozo Na. FA.130/170/01/5 uliotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tarehe 22 Januari 2021, Benki

hazitakiwi kuzidi kiasi cha mikopo chechefu kwa zaidi ya asilimia 5. Pamoja na ukomo huu uliowekwa lakini uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa na mikopo chechefu ya asilimia 21.50 kufikia tarehe 31 Desemba 2023 na mwaka 2022 mikopo chechefu ilikuwa asilimia 20.28. Kiwango kikubwa cha mikopo chechefu kinaendelea kuzorotesha mtaji wa benki.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2021 inaeleza kuwa taasisi ya fedha ya maendeleo itaanza kufanya kazi ikiwa wakati wote ina mtaji wa msingi usiopungua shilingi bilioni 200 au zaidi ya kiasi hicho. Hata hivyo, Benki ya Maendeleo TIB hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2023 ilikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 88.12 ambao ni chini ya mahitaji ya mtaji wa shilingi bilioni 200, hivyo kuwa na upungufu wa mtaji wa shilingi bilioni 111.88 sawa na asilimia 127. Hali hii ina athiri utendaji wa benki hii kwa kiasi kikubwa na kusababisha hatari kwa Benki kupoteza sifa zake za kujiendesha na inaweza kusababisha Benki kuwekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, benki ya Maendeleo TIB ni benki za Serikali na ilianzishwa kimkakati ili iweze kuwezesha upatikanaji wa mitaji ya muda mrefu na wa kati kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kusimamia mifuko maalum kama itakavyohitajiwa na Serikali. Benki hii ni ya kimakakati ila hali yake si yakuridhisha na kama jitihada za makusudi hazitachukuliwa benki hii itabidi kuwekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu Tanzania (BOT), ni rai ya Kamati kuwa Serikali ikahakikisha inaisimamia na kuiwezesha kikamilifu benki hii ili iweze kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

2.5.4 Baadhi ya Miradi ya Uwekezaji kuanza kabla ya kukamilika kwa maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mradi

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia mashirika na taasisi za umma imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji inayolengwa kutoa huduma kwa jamii au inayokusudiwa kuongeza ufanisi katika utendaji wa shirika au taasisi husika. Ili kupata tija ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika miradi mbalimbali ya maendeleo ni muhimu miradi hii ikakamilika na kuweza kuanza kutumika kwa wakati.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, baadhi ya miradi ya maendeleo imekuwa ikianzishwa bila kukamilisha maandalizi yote ya msingi ikwemo kufanya upekuzi wa kina wa wakandarasi na kufanya maandalizi ya fedha jambo ambalo limekwamisha miradi hii ya uwekezaji kuweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya miradi ya maendeleo utekelezaji wake umechukua muda mrefu kutokana na kutopatikana kwa fedha za utekelezaji kwa wakati. Aidha, kwa baadhi ya miradi, taasisi/shirika la umma zimekuwa zinasaini mkataba wa utekelezaji na Wakandarasi kabla ya kukamilisha maandalizi ya fedha hivyo kupelekea mradi kuchelewa kuanza na hivyo unasababisha kuzalishwa kwa riba za uchelelweshaji na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji wa mradi.

Vile vile, Kamati ilibaini, kuna baadhi ya miradi imeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na wakandarasi waliokabidhiwa mradi kutokuwa na sifa za kutosha. Mfano ni Mradi wa ujenzi wa vituo vya pamoja vya vya ukaguzi vya Manyoni na Nyakanazi unaotekelezwa na Wizara ya Fedha na kusimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kupitia fedha za ufadhili takribani shilingi EURO19,215,328 ambapo ufadhili huu ulitoka Nchi za

Umoja wa Ulaya na malipo yalifanyika kwa kuzingatia hatua za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi alikabidhiwa mkandarasi *M/S Impresa di Costruzio Ing. E Montovani S.p.A co socio Via Belgio* ambaye alifilisika miaka miwili (2) mara baada ya kukabidhiwa mradi. Mkandarasi huyu alitekeleza mradi huu kwa asilimia 60 (Manyoni) na asilimia 50 (Nyakanazi).

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya jambo hili ni kuwa mkandarasi huyu hakufanyiwa upekuzi wa kina ili kubaini uwezo wake halisi hususani kipengele cha uwezo wa kifedha. Matokeo yake ni mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi yake kwa wakati na pia kufilisika hivyo hataweza kukamilisha kazi yake. Aidha, jambo hili limesababisha msaada uliokuwa umepatikana kwa ajili ya kutekeleza miradi hii kukoma (kusitishwa) kwa kuwa malipo (disbusment of fund) yalitegemea hatua za utekelezaji, kwa hiyo kufilisika kwake kumepelekea kusitishwa kwa msaada na hivyo miradi hii imesimama kwa takribani miaka sita sasa.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa kwa taasisi zinazotekeleza miradi ya uwekezaji ni vema zifanye maandalizi yote ya awali ikiwemo kujiridhisha juu ya upatikanaji wa fedha, upekuzi wa wakandarasi na uzingatiaji wa mikataba ya utekelezaji wa miradi kwa lengo la kuhakikisha miradi wanayotekeleza inakamilika kwa wakati bila nyongeza yoyote ya gharama ili tija ya uwekezaji katika mradi husika kuweza kupatikana na kuiepusha Serikali na mizigo ya gharama zisizo za msingi zinazotokana na riba.

2.5.5 Gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya vijiji-miji

Mheshimiwa Spika, Nishati ya Umeme ni miongoni mwa huduma muhimu kwakuwa husaidia kufungua fursa na kuchochea maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na za kiuchumi, kijamii, kiteknolojia n.k katika

taifa. Kwasasa Serikali inaendelea na mpango wake wa kutekeleza mradi wa kuunganisha umeme vijijini kupitia Mradi wa Uwekezaji wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (Turnkey Phase III Round II).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa ya uwekezaji ya Wakala wa Nishati vijijini kwa lengo la kubaini ufanisi wa shughuli unaozitekeleza, Kamati ilibaini kuwa kwa kiasi kikubwa wakala imetekeleza jukumu lake ambapo kwa kipindi ambacho tunakitolea taarifa ya ujumla ya vijiji 10,377 vilikuwa vimefikishiwa miundombinu ya umeme kati ya vijiji 12,318 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 84.24.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati uliibaini kuwa tija ya uwekezaji katika miradi ya REA ni ndogo katika maeneo yenye mwonekano wa vijiji-miji kwani uwekezaji uliofanywa wa kusambaza huduma katika maeneo hayo imekuwa kubwa ikilinganishwa na kasi ya uunganishaji wa wananchi katika maeneo hayo kutokana na uwezo mdogo wa vipato vya jamii ya maeneo hayo ambao nao wanatozwa gharama sawa na maeneo yenye hadhi za miji au majiji. Hali hii inasababisha wanachi wa maeneo hayo washindwe kuunganisha umeme hivyo kushusha ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika sekta kwani ni watu wacheche sana wanaojiunga katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia jambo hili Kamati ilielezwa kuwa, Serikali inaendelea na mchakato wa kutathmini bei halisi na stahiki zinazopaswa kutozwa katika maeneo yenye sifa hizo ili kuwezesha walengwa kuweza kujiunga na huduma ya umeme kulingana na uwezo wao halisi wa kipato na kiuchumi. Pamoja na maelezo yaliyotolewa Serikali, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mchakato huo umechukua muda mrefu jambo linaloendelea kuathiri ufanisi wa mtaji na kushusha tija ya uwekezaji iliyofanywa na Serikali kwenye miradi ya REA kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamaoni kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Mamlaka zake zinazohusika ihakikishe inaharakisha na kukamilisha tathmini za gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya namna hiyo ili kuongeza ufanisi wa mtaji na tija ya uwekezaji lakini pia kufanikisha azma ya Serikali ya kupeleka nishati bora vijijini kwa madhumuni ya kukuza Uchumi na kuboresha hali za Maisha za wanachi wa vijijini iweze kutimia.

2.5.6 Ujenzi na Uendeshaji wa Stendi ya Msamvu – Morogoro

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Msamvu Properties Company (T) Limited ilianzishwa mwezi Septemba 2009 kwa ubia kati ya uliokuwa Mfuko wa LAPF na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ikiwa na dhumuni la kusimamia ujenzi na uendeshaji wa mradi wa kituo cha mabasi cha Msamvu. Makubaliano ya msingi ya utekelezaji wa mradi huu yalikuwa ni Manispaa kutoa ardhi kwa ajili ya mradi kama mchango wao na Mfuko kutoa fedha za kugharamia ujenzi, gharama za mshauri mwelekezi na gharama nyingine za mradi zitakazoidhinishwa na wabia.

Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la Mfuko kushiriki uwekezaji huu lilikuwa ni kupata faida ya uwekezaji ili kuongeza thamani ya michango ya wanachama wa Mfuko na kuongeza mapato kwa Manispaa ya Morogoro. Mradi pia ulilenga kuboresha miundombinu ya usafiri hususan stendi kwa Mkoa wa Morogoro. Gharama zilizotumiwa na Mfuko katika utekelezaji wa mradi huu ni shilingi bilioni 14.76.

Baada ya kukamilika kwa gharama za ujenzi kutokana na taarifa ya fedha zilizotumika (*Final accounts)* ilikubalika Mfuko umiliki asilimia 74 na Halmashauri asilimia 26 kulingana na mchango wa kila mbia katika mradi ambapo Kampuni itaendesha mradi na wanahisa watapata faida yao kwa mujibu wa hisa za umiliki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 Serikali iliukabidhi mradi huu kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa ahadi kuwa fedha za uwekezaji huu zitarejeshwa na Serikali. Mfuko umekuwa ukifuatatilia urejeshwaji wa fedha ulizowekeza katika mradi huo bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, Kulingana na upembuzi yakinifu uliofanyika wakati wa kuanza mradi ulionesha kwamba gharama za mradi zingeweza kurejeshwa katika kipindi cha miaka 13 ambapo wastani wa mapato ya mradi kwa mwaka ilikuwa shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa Mfuko uliwekeza fedha ambazo ni sehemu ya michango ya wanachama wake. Kamatiinamaoni kuwa ufumbuzi wa suala hili ni lazima upatikane kwa manufaa ya pande zote mbili yani Mfuko wa PSSSF na Halmashauri ya Manispaa ya Msamvu.

2.5.7 Changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mwaka 2014 (The VAT Act 2014 [CAP.148 R.E. 2019]) kwenye Kampuni za Madini kwa Soko la Ndani

Mheshimiwa Spika, Taasisi zinazofanya biashara katika sekta ya madini nchini zimekuwa zikitekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Sheria, taratibu na miongozo ya kodi nchini. Sheria zinazotumiwa katika masuala ya kodi ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (The VAT Act [CAP.148 R.E. 2019]) na Sheria ya Kodi ya Mapato (The Income Tax Act [CAP. 332 R.E 2019]).

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika tasnia hii ulibaini uwepo wa changamoto zinazotokana na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. Sheria hii inatoa fursa ya msamaha wa kodi hii (VAT exemption) kwa kampuni zinazoingiza madini nchini (*refined and raw minerals*) na kwa wachimbaji wadogo (*Small Scale Miners*). Vilevile, sheria inatoa msamaha wa kodi ya VAT kwa kampuni zinazouza madini nje ya nchi.

Wakati sheria hii inazitaka kampuni zinazoendesha shughuli za biashara hiyo ndani ya nchi kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Hali hii inaathiri kampuni za ndani zinazotegemea soko la ndani katika kuendesha biashara zake kwani zinakutana na ushindani mkubwa wa bei sokoni kwakuwa hulazimika kuuza kwa bei ya juu ili kuweza kufidia kiasi cha VAT wanacholipa pamoja na kupata faida. Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) kupitia kampuni tanzu yake ya STAMIGOLD ni moja ya kampuni iliyobainika kukumbwa na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha taasisi zinazoendesha shughuli za madini ndani ya nchi zinajiendesha kwa ufanisi na kuweza kushindana katika soko ni muhimu Serikali ikafanya mapitio ya Sheria ya kodi ya Ongezeko la thamani kwa lengo la kuhakikisha inakidhi mahitaji ya kibiashara kwa taasisi zote za madini kwa kuweka uwiano wenye kuzipa fursa sawa ya ushindani na kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hali itakayoipa nafasi ya kukua na kujiimarisha kimtaji na hatimaye Serikali kupata tija inayokusudiwa.

2.5.8 Vigezo vya Utendaji vilivyowekwa na Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 10 (2) (d) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370, Ofisi ya Msajili wa Hazina inatakiwa kuweka vigezo vya utendaji kwenye mashirika, taasisi na wakala za Serikali kwa lengo la kupima utendaji na kuhakikisha tija ya uwekezaji katika mashirika na taasisi hizo inapatikana

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kuchambua taarifa za utendaji wa mashirika yaliyofika mbele yake kwa kulinganisha na viashiria vya utendaji vilivyowekwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Vigezo vya utendaji wa mashirika vinajumuisha kiwango cha ukuaji wa mapato, Uwiano wa Gharama za Uendeshaji kwa mapato, Uwiano wa Madeni na Mali, uwiano wa madeni na mtaji, ukwasi wa shirika n.k.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya mashirika yamekuwa yakijiendesha nje ya vigezo vilivyopangwa na hivyo kuathiri utendaji pamoja na tija ya uwekezaji kwa mashirika husika. Vigezo vilivyozingatiwa sana na Kamati wakati wa uchambuzi ni pamoja na kigezo cha uwiano wa gharama za uendeshaji kwa mapato. Kigezo hiki kinapima uwezo wa mapato kugharamia shughuli za shirika katika mwaka husika. Kamati ilibaini kuwa matumizi kwa baadhi ya mashirika yamekuwa kwa kasi kubwa kuliko kasi ya ukuaji wa mapato hivyo kusababisha mashirika na taasisi nyingi kutengeneza hasara/nakisi au kubaki na fedha za ziada kwa ajili ya kufanya uwekezaji. Hii inaonesha kwamba mashirika na taasisi nyingi zinazalisha mapato kwa ajili ya kutumia tu na sio kufikiria namna ambavyo yanaweza kufanya uwekezaji utakaosaidia kukua na kuimarisha utendaji wa taasisi hizo kwa siku za baadaye. Taasisi zilizokuwa na changamoto hii ni pamoja na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Bodi ya Mkonge (TSB), Shirika la Reli (TRC), Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), TIB Rasilimali, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA).

Kigezo kingine kilichozingatiwa na Kamati ni kigezo cha Uwiano wa mali za muda mfupi kwa madeni ya muda mfupi, uwiano huu unalenga kupima uwezo wa taasisi kulipa madeni ya muda mfupi pale ambapo atahitajika kufanya hivyo kwa kutumia mali zake za muda mfupi. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mashirika taasisi na mashirika mengi ya umma yamekuwa hayakidhi kigezo hili jambo ambalo limepelekea madeni makubwa na mengine yamezalisha riba za ucheleweshaji. Miongoni mwa mashirika hayo ni pamoja na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Shirika la Reli (TRC), Watumishi Housing Investment (WHI), Usafiri Dar es Salaam Rapid Transit (U-DART), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Bodi ya Usimamizi Stakabadhi Ghalani (WRRB).

Mheshimiwa Spika, kigezo kingine ni Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini, kwa kuzingatia kigezo hiki Mashirika ya umma yanapaswa kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali mwaka hadi mwaka. Uchambuzi wa Kamati umebaini ni mashirika machache sana yaliyoweza kufikia kigezo, lakini baadhi ya mashirika tena yakiwa na fursa ya kufanya vizuri lakini bado yanapokea ruzuku ya Serikali. Kwa mfano; Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Wakala wa Umeme na Ufundi (TEMESA) na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali za kutafuta fedha za kuwekeza katika taasisi na mashirika ya umma, ni vema kuimarisha usimamizi wa mashirika ya umma kwa kuhakikisha wanatekeleza kikamilifu vigezo vyote vya utendaji walivyopatiwa na Msajili wa Hazina.

2.5.9 Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

Mheshimiwa Spika, Jukumu la mamlaka za hifadhi ni Kuendeleza uhifadhi wa maliasili na malikale pamoja na kuendeleza utalii. Utekelezaji wa majukumu haya ni moja ya sababu inayopelekea kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii nchini. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka hizi zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya utekelelazaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kufuatia janga la UVIKO-19, Taasisi za NCAA na TANAPA ziliathirika ikiwa ni matokeo ya athari za janga hilo, na hivyo Serikali katika kunusuru uendeshaji wa Taasisi hizo ilifanya marejeo ya ukusanyaji mapato na kuanza kuzipa ruzuku Taasisi hizi katika kipindi ambacho sekta ya utalii ilikuwa imeathirika.

Aidha, kutokana na kurejea kwa utalii kwa nguvu zilizowekwa na Serikali ikiongozwa na Rais wa JMT, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, idadi ya watalii imeongezeka na hivyo, Taasisi hizi sasa kwa mapato ambayo yanakusanywa zinaweza kujitegemea kujiendesha lakini bado zinaendelea kwenye utaratibu makusanyo yao kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wao kupokea ruzuku kwa ajili ya kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, awali taasisi ya NCAA na TANAPA waliweza kukusanya mapato yao na kuyatumia kwa ajili ya utekelelzaji wa shughuli mbalimbali za Mamlaka ikiwemo kuboresha miundombinu kwa wakati pindi inapohitajika na kufanikisha utekelezaji wa jukumu zima la utalii na kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria. Kutokana na mabadiliko yaliyofanywa kutokana na athari za UVICO-19 Mamlaka hizi zinalazimika kusubiri mgao wa ruzuku kutoka Serikalini jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limekwamisha utendaji wa Mamlaka kwani fedha hizi zimekuwa haziendi kwa wakati stahiki (misimu ya utalii kuanzia mwezi Julai hadi Septemba) lakini pia bajeti wanazotengewa zimekuwa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mamlaka jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu yake hususani miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ufinyu huu wa bajeti pamoja na ucheleweshaji wa fedha kwa taasisi hizi umeathiri pia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa upande wa NCAA athari za ucheleweshaji wa fedha za miradi zimepelekea wakandarasi kudai riba za ucheleweshaji kwa miradi miwili (ujenzi wa jengo la Makao makuu ya Mamlaka pamoja na ujenzi wa Barabara ya View Point) kiasi cha jumla ya shilingi milioni 219.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa mapato halisi yatokanayo na shughuli za utalii katika hifadhi hizi ni makubwa lakini bajeti inayoidhinishwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za hifadhi hizi ni ndogo

haiakisi mahitaji halisi ya malmaka hizi jambo linaloathiri utendaji kazi wa hifadhi hizi. Aidha, Kamati imebaini kuwa changamoto ya miundombinu ya Barabara pamoja na vyoo imekuwa kikwazo kwa watalii hususani watalii kutoka nje ya nchi jambo linaloa idadi ya *returning visitors* hivyo kuathiri mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, taasisi za NCAA na TANAPA ni kati ya taasisi ambazo zilikuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa katika mfuko Mkuu wa Serikali kabla ya kuathiriwa na janga la UVICO -19, Juhudi kubwa za Serikali zimefanyika na hatimaye taasisi hizi zimeweza kurudi katika hali ya awali ya uzalishaji wa mapato licha ya kukabiliwa na changamoto zilizobainishwa hapo juu. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali kutafakari ufumbuzi wa jambo hili na taasisi hizi za kimkakati kuruhusiwa kukusanya mapato yake ili ziweze kuwa na ukwasi muda wote na kuwawezesha kutekeleza majukumu yake hususani jukumu la ujenzi na ukarabati wa miundombinu za mamlaka ili kuziwezesha kuwa na ufanisi na kuweza kuhudumia watalii kwa ufanisi zaidi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni tegemeo la Bunge katika kufuatilia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Serikali kwa lengo la kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuisimami na Kuishauri Serikali kuhusu uwekezaji inaoufanya na Serikali. Kutokana na uchambuzi na ufuatiliaji uliofanywa na Kamati, yapo mambo yanayotolewa maoni na mapendekezo kwa madhumuni ya kulisaidia Bunge kujadili na kuamua. Kwa ujumla mambo makuu yanayojitokeza katika Taarifa hii ni pamoja na:-

i) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambako Serikali imewekeza mtaji wa Umma na kuwa na mategemeo kupata faida kupitia mtaji huo zimekuwa hazichangii kabisa na nyingine zinachangia kidogo kuliko zinavyopaswa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

ii) Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikali kwa Taasisi na Mashirika ya Umma umeendelea kuongezeka badala ya kupungua kama inavyobainishwa katika vigezo vya utendaji wanavyopewa Bodi na Menejimenti za Mashitrika ya Umma;

iii) Ufanisi wa utendaji wa baadhi ya taasisi na Mashirika ya Umma umekuwa sio wa kuridhisha jambo ambalo linaathiria Mtaji wa Umma uliowekezwa na Serikali katika taasisi na mashirika husika;

iv) Changamoto ya Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB inavyoathiri utendaji wa Benki hii muhimu;

v) Namna ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi inavyoongezea Serikali gharama za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, baadhi ya miradi kukwama kutokana na wakandarasi wasiokuwa na sifa kupewa miradi ya uwekezaji hivyo kupelekea miradi hiyo kutokamilika kwa wakati au kusimama kwa muda mrefu;

vi) Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) inayotokana na ufinyu wa bajeti ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizi; na

vii) Namna Mfuko wa PSSSF unavyokosa tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma uliowekezwa katika mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Msamvu; na

viii) Tija hafifu ya uwekezaji wa mtaji wa umma kwa miradi ya REA katika maeneo ya vijiji-miji kutokana na wakazi wa maeneo hayo kushindwa kumudu gharama za kuunganisha umeme;

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, kwa msingi wa uchambuzi ulikofanywa na Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati ambayo kwa maoni ya Kamati, iwapo Bunge litaridhia yanakusudia kutatua changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma na hatimaye kuongeza ufanisi wa Uwekezaji mkubwa uliofanya na unaoendelea kufanywa na Serikali.

3.2.1 Uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali

KWA KUWA, Sheria ya Msajili wa Hazina madaraka na majukumu sura 370 Kifungu Na. 8 (i) (f) pamoja na sheria ya Makampuni kifungu

cha 180 kinazitaka Taasisi na Mashirika ya umma kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia sheria hizo;

NA KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamekuwa hayatekelezi takwa hili la sheria hivyo kupelekea kuchangia kidogo au kutokuchangia kabisa katika mfuko Mkuu wa Serikali hivyo kuinyima Serikali mapato stahiki;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:

i) Serikali iweke utaratibu wa kuziwajibisha Bodi na Menejimenti za Taasisi na Mashirika ya Umma yanayoshindwa kutekeleza kigezo hiki cha kisheria cha kuchangia katika mfuko Mkuu wa Serikali.

ii) Serikali kupitia Msajili wa Hazina iongeze usimamizi kwa Taasisi na Mashirika ya umma kuhakikisha yanaimarisha utendaji wake kwa lengo la kuongeza mapato yake na kuongeza mchango wake katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

3.2.2 Utegemezi wa Ruzuku kutoka Serikalini

KWA KUWA, moja ya kigezo cha utendaji kilichowekwa kwa Taasisi na Mashirika ya Umma ni kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali mwaka hadi mwaka ili baadae yaweze kujitegemea;

NA KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamekuwa yakiongeza kiwango cha utegemezi wa ruzuku badala ya kupunguza kama kigezo kinavyoelekeza;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

i) kufanya upembuzi wa Mashirika yanayotegemea ruzuku na kuyawekea mipango ya kupunguza utegemezi hususani katika kipengele cha mishahara na matumizi mengineyo (OC); na

ii) kusimamia Taasisi na Mashirika ya umma yanayotegemea ruzuku kuhakikisha yanatafuta njia mbadala za kupata rasilimali ikiwemo kutumia mikopo nafuu na kushirikisha sekta binafsi (Public Private Partnership-PPP) katika utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ya kibiashara ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

3.2.3 Tathimini ya utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma

KWA KUWA, imebainika kuwa kuna baadhi ya taasisi na mashirika ya umma utendaji wake unasua sua, jambo ambalo linaathiri tija ya uwekezaji wa mtaji wa umma;

NA KWA KUWA, miongoni mwa changammoto zinazopelekea kusuasua kwa utendaji huo ni pamoja na

i) Upungufu wa mtaji wa uendeshaji
ii) Kupata hasara/nakisi kwa miaka mitatu mfululizo;
iii) Kushindwa kutumia kikamilifu fursa za uwekezaji zilizopo
iv) Mchakato wa sheria ya manunuzi
v) Mchakato wa kupata vibali vya ajira; na
vi) Mchakato wa kupata vibali vya mikopo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kufanya mapitio ya Taaasisi na Mashirika ya umma kwa lengo la kubainisha changamoto wanazokabiliana nazo na kuwa na mpango mahususi wa kutatua changamoto hizo ili taasisi husika ziweze kuongeza ufanisi wake na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

3.2.4 Upungufu wa Mtaji kwa Benki ya Maendeleo TIB

KWA KUWA, Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za benki na Taasisi za Fedha za mwaka 2021 inaeleza kuwa taasisi ya fedha ya maendeleo itaanza

kufanya kazi ikiwa wakati wote ina mtaji wa msingi usiopungua shilingi bilioni 200 au zaidi ya kiasi hicho;

NA KWA KUWA, Benki ya Maendeleo TIB imebainika kuwa na kiasi cha mtaji pungufu ya kigezo kilichowekwa hivyo kuathiri utendaji wake;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuongeza mtaji kwa benki ya maendeleo TIB ili kukidhi matakwa ya sheria ya Benki Kuu (BOT) na kumudu ushindani kwenye soko kwani ni muhimu benki hii ikaendelea kuwepo ili itekeleze malengo ya uanzishwaji wake.

3.2.5 Ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi

KWA KUWA, imebainika kwa baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yamekuwa yakianza utekelezaji wa miradi kabla ya kukamilisha maandalizi ya awali ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji.

NA KWA KUWA, kitendo hiki kimepelekea kuongeza gharama za utekelezaji wa mradi zinazotokana na riba ya ucheleweshaji;

NA KWA KUWA, ucheleweshaji wa malipo umewaathiri pia baadhi ya wakandarasi hasa wazawa ambao mitaji yao ni midogo hivyo kupelekea kudumaa kiutendaji na kukosa sifa za kupata miradi mingine;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Msajili wa Hazina kusimamia kikamilifu taaasisi na mashirika ya umma kuhakikisha wanakamilisha maandalizi yote ya awali kabla ya kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi husika kwa lengo la kuepusha kuiongezea Serikali mzigo utokanao na ulipaji wa riba za ucheleweshaji.

3.2.6 Wakandarasi wasiokuwa na vigezo kupewa kazi za utekelezaji wa miradi.

KWA KUWA, moja ya kigezo cha kupata wakandarasi wa kutekeleza miradi ya maendeleo ni kufanya upekuzi kwa lengo la kubaini uwezo wa wakandarasi husika

NA KWA KUWA, imebainika kuna Baadhi ya miradi ya uwekezaji imetolewa kwa wakandarasi ambao hawana sifa jambo linaloathiri uwekezaji wa utekelezaji wa mradi na kupelekea tija ya uwekezaji kuchelewa. Mfano mradi wa ujenzi wa kituo cha pamoja cha Manyoni na Nyakanazi;

NA KWA KUWA, moja ya jukumu la Msajili wa hazina ni kusimamia uwekezaji unaofanya na taasisi na Mashirika ya Umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali isimamie kikamilifu taasisi na mashirika ya umma yanayotekeleza miradi ya uwekezaji ili kuhakikisha yanafanya upekuzi wa kina na kujiridhisha juu ya uwezo wa wakandarasi wanaokabidhiwa miradi hiyo kwa lengo la kujiepusha na changamoto katika utekelezaji wa miradi hiyo ikiwemo changamoto ya miradi kutokamilika kwa wakati.

3.2.7 Gharama za kuunganisha umeme kwa maeneo ya vijiji – miji

KWA KUWA, gharama za uunganishaji umeme inayotozwa kwa maeneo ya vijiji – miji imesababisha kasi ya wananchi wa maeneo hayo kuunganisha umeme kuwa ndogo ukilinganisha na kasi ya usambazaji wa miundombinu ya umeme katika maeneo;

NA KWA KUWA, kasi ndogo hii inafifisha tija ya uwekezaji mkubwa uliofanya na Serikali katika kujenga miundombinu hii na pia tija ya uanzishaji wa REA;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Mamlaka zake zinazohusika ihakikishe inaharakisha kukamilisha tathmini za gharama za kuunganisha umeme katika maeneo ya namna hiyo na kubainisha majina ya maeneo na gharama ndani ya miezi sita ili kuongeza ufanisi wa mtaji uliowekezwa katika miradi hii. Jambo hili litapelekea kukamilisha azma ya Serikali ya kupeleka nishati ya gharama nafuu vijijini kwa lengo la kukuza Uchumi na kuboredha hali ya maisha ya wanachi wa vijijini.

3.2.8 Uzingatiaji wa vigezo vya utendaji vilivyowekwa na Msajili wa hazina

KWA KUWA, kifungu cha 10(2) (d)cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 (Madaraka na Majukumu) kinamuelekeza Msajili wa Hazina kupanga vigezo vya utendaji kwa Taasisi na Mashirika ya umma;

NA KWA KUWA, Msajili wa Hazina amepanga vigezo hivyo lakini

i) Baadhi ya vigezo ni vya jumla haviakisi uhalisia wa majukumu ya Taasisi au Shirika husika;
ii) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamekuwa yakijiendesha nje ya vigezo vya utendaji vilivyopangwa licha ya kuwa vigezo hivyo vinaendana na uhalisia wa majukumu ya taasisi zao.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba,

i) Msajili wa Hazina afanye marejeo ya vigezo vya utendaji na kuvipanga kwa Taasisi kwa kulingana na uhalisia wa majukumu ya Taasisi au Shirika husika

ii) Kuzisimamia Taasisi na Mashirika ya umma kuhakikisha zinajiendesha ndani ya vigezo vya utendaji ilivyopatiwa kwa lengo la kuleta ufanisi na tija ya uwekezaji kuweza kupatikana.

iii) Kuweka utaratibu wa kuwachukulia hatua stahiki Bodi na Menejimenti za Taasisi zinazoshindwa kutekeleza vigezo vya utendaji walivyopatiwa.

3.2.9 Changamoto katika utendaji wa Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

KWA KUWA, nia ya Serikali kufanya marejeo ya ukusanyaji mapato ya Taasisi za NCAA na TANAPA na kuanza kuzipa ruzuku Taasisi hizi katika kipindi ambacho sekta ya utalii ilikuwa imeathirika ilikuwa ni kunusuru uendeshaji wa Taasisi hizo kutokana na athari ya janga la UVIKO-19;

NA KWA KUWA, juhudi kubwa zikiongozwa na Rais wa JMT, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimechangia kurejea kwa sekta ya utalii na idadi ya watalii imeongezeka na hivyo, Taasisi hizi sasa kwa mapato ambayo yanakusanywa zinaweza kujitegemea kujiendesha

NA KWA KUWA, bajeti inayotengwa kwa taasisi hizi haziendani na mahitaji halisi ya taasisi hizi na pia fedha zinazotengwa hazipelekwi kwa wakati hivyo kuathiri utendaji wake

KWA HIYO BASI, Bunge linaazima kwamba, Serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa taasisi ya NCAA na TANAPA kukusanya mapato yake kwa lengo la kuwawezesha kuwa na ukwazi muda wote ili waweze kufanya maendeleo ya maeneo wanayosimamia kwa wakati na kuongeza ufanisi wa Taasisi muhimu katika Tasnia ya Maliasili na Utalii.

3.2.10 Ujenzi na uendeshaji wa Stendi ya Msamvu

KWA KUWA, Mfuko wa PSSSF uliwekeza jumla ya shilingi 14.76 katika mradi wa ujenzi wa Stendi ya Msamvu fedha ambazo ni sehemu ya michango ya wanachama wake,

NA KWAKUWA, mwaka 2018 Serikali ilifanya maamuzi ya kuhamishia uendeshaji wa stendi ya Msamvu kwa Halmashauri ya Manisapaa ya Morogoro kwa ahadi kwamba Serikali itairejeshea PSSSF fedha ilizowekeza katika mradi huu lakini ahadi hii haijatekelezwa kwa takribani miaka sita sasa;

KWA HIYI BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali irudishe uendeshaji wa stendi ya Msamvu kwa Mfuko wa PSSSF ili mradi husika utumike kurejesha gharama za uwekezaji na baada ya Mfuko kurudisha gharama za uwekezaji stendi itarejea kuwa mali ya Manispaa ya Morogoro. Jambo hili pia litaipunguzia Serikali mzigo wa kulipa gharama za uwekezaji zilizotolewa na Mfuko wa PSSSF.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo, ushauri na miongozo ya kiti chako kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa madhumuni ya kupata tija ya uwekezaji na kuboresha ustawi wa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamatihii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamatina kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Augustine Vumma Hole, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mary Masanya, Mb
3. Mhe. Abbas Gulam Tarimba, Mb
4. Mhe. Aeshi Alfan Hillary, Mb
5. Mhe. Aida Joseph Kenani, Mb
6. Mhe. Angelah Jasmin Kairuki, Mb

7. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb
8. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb
9. Mhe. Bonah Ladislaus Kamoli, Mb
10. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
11. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb
12. Mhe. Deonatus Philip Mwanyika, Mb
13. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb-
14. Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb
15. Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
16. Mhe. Fratey Gregory Massay Mb
17. Mhe. George Natany Malima, Mb
18. Mhe. Haji Amour Haji, Mb
19. Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb
20. Mhe. Matha Nehemia Gwau, Mb
21. Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb
22. Mhe. Santiel Erick Kirumba, Mb
23. Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb

Mheshimiwa Spika, Vilevile, napenda kuishukuru Ofisi ya Msajili wa Hazina inayoongozwa na Ndugu Nehemia Mchechu kwa ushirikiano wa dhati mlioutoa kwa Kamatina kushauri namna bora ya kuwezesha Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake kwa lengo la kuleta tija kwa Taifa na kupata chumo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Ildephonce Leonard

kwa ushirikiano wa hali ya juu walioutoa ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamatikutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati mpaka sasa ninapowasilisha taarifa hii ya Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamatiyanalenga kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo uwe wa ufanisi na ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako sasa likubali kupokea Taarifa ya Kamatiya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji

wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, na kuijadili ili kuamua na kuiwezesha Serikali kuyafanyia kazi maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Augustine Vuma Hole, Mb.

MWENYEKITI

KAMATIYA KUDUMU YA BUNGE YA

UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC)

29 Oktoba, 2024

1.0 KIAMBATISHO 01: ORODHA YA UWEKEZAJI WA SERIKALI KWENYE MASHIRIKA NA TAASISI ZA UMMA (PSCS)

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
I: Mashirika ya Umma - 35					
1.	Air Tanzania Company Limited	ATCL	100	Ndani ya nchi	Biashara
2.	Arusha International Conference Centre	AICC	100	Ndani ya nchi	Biashara
3.	Cereals and Other Produce Board	CPB	100	Ndani ya nchi	Biashara
4.	Cooperative Audit And Supervision Corporation	COASCO	100	Ndani ya nchi	Biashara
5.	Kariakoo Market Corporation	KMC	49	Ndani ya nchi	Biashara
6.	Kilimanjaro Airports Development Company	KADCO	100	Ndani ya nchi	Biashara
7.	Marine Services Company Limited	MSCL	100	Ndani ya nchi	Biashara
8.	Medical Stores Department	MSD	100	Ndani ya nchi	Biashara
9.	Mzinga Corporation	MZINGA	100	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
10.	National Development Corporation	NDC	100	Ndani ya nchi	Biashara
11.	National Housing Corporation	NHC	100	Ndani ya nchi	Biashara
12.	National Insurance Corporation	NIC	100	Ndani ya nchi	Biashara
13.	National Ranching Company	NARCO	100	Ndani ya nchi	Biashara
14.	National Service Corporation Sole	SUMA JKT	100	Ndani ya nchi	Biashara
15.	Ngorongoro Conservation Area Authority	NCAA	100	Ndani ya nchi	Biashara
16.	Prisons Corporation Sole	SHIMA	100	Ndani ya nchi	Biashara
17.	Self Microfinance Fund	SELF MF	100	Ndani ya nchi	Biashara
18.	State Mining Corporation	STAMICO	100	Ndani ya nchi	Biashara
19.	Tanzania Agricultural Development Bank Limited	TADB	100	Ndani ya nchi	Biashara
20.	Tanzania Automotive Technology Centre	TATC NYUMBU	100	Ndani ya nchi	Biashara
21.	Tanzania Brodcasting Corporation	TBC	100	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
22.	Tanzania Commercial Bank	TCB BANK	83	Ndani ya nchi	Biashara
23.	Tanzania Electric Supply Company Limited	TANESCO	100	Ndani ya nchi	Biashara
24.	Tanzania Fertilizer Company	TFC	100	Ndani ya nchi	Biashara
25.	Tanzania Mercantile Exchange Plc	TMX	67	Ndani ya nchi	Biashara
26.	Tanzania National Parks	TANAPA	100	Ndani ya nchi	Biashara
27.	Tanzania Petroleum Development Corporation	TPDC	100	Ndani ya nchi	Biashara
28.	Tanzania Police Force Corporation Sole	TPFCS	100	Ndani ya nchi	Biashara
29.	Tanzania Ports Authority	TPA	100	Ndani ya nchi	Biashara
30.	Tanzania Posts Corporation	TPC	100	Ndani ya nchi	Biashara
31.	Tanzania Railways Corporation	TRC	100	Ndani ya nchi	Biashara
32.	Tanzania Standard Newspapers Limited	TSN	100	Ndani ya nchi	Biashara
33.	Tanzania Telecommunications	TTCL	100	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Corporation				
34.	TIB Development Bank	TIB DFI	100	Ndani ya nchi	Biashara
35.	Utt Asset Management And Investor Services	UTT AMIS	100	Ndani ya nchi	Biashara
II: Elimu ya Juu, Utafiti na Mafunzo Stadi – 74					
1.	Agency for the Development of Educational Management	ADEM	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Ardhi Institute Morogoro	ARIMO	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Ardhi University	ARU	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Arusha Technical College	ATC	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Mozambique-Tanzania Centre for Foreign Relations	CFR	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	College of African Wildlife Management	CAWM	100	Ndani ya nchi	Huduma
7.	College of Business Education	CBE	100	Ndani ya nchi	Huduma
8.	Dar es Salaam Institute of Technology	DIT	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
9.	Dar es Salaam Maritime Institute	DMI	100	Ndani ya nchi	Huduma
10.	Dar es Salaam University College of Education	DUCE	100	Ndani ya nchi	Huduma
11.	East African Statistical Training Centre	EASTC	100	Ndani ya nchi	Huduma
12.	Fisheries Education and Training Agency	FETA	100	Ndani ya nchi	Huduma
13.	Institute of Accountancy Arusha	IAA	100	Ndani ya nchi	Huduma
14.	Institute of Adult Education	IAE	100	Ndani ya nchi	Huduma
15.	Institute of Finance Management	IFM	100	Ndani ya nchi	Huduma
16.	Institute of Judicial Administration Lushoto	IJA	100	Ndani ya nchi	Huduma
17.	Institute of Rural Development Planning	IRDP	100	Ndani ya nchi	Huduma
18.	Institute of Social Works	ISW	100	Ndani ya nchi	Huduma
19.	Kibaha Education Centre	KEC	100	Ndani ya nchi	Huduma
20.	Livestock Training Agency	LITA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
21.	Local Government Training Institute	LGTI HOMBOLO	100	Ndani ya nchi	Huduma
22.	Mbeya University Of Science And Technology	MUST	100	Ndani ya nchi	Huduma
23.	Mkwawa University College of Education	MUCE	100	Ndani ya nchi	Huduma
24.	Moshi Co-operative University	MOCU	100	Ndani ya nchi	Huduma
25.	Muhimbili University of Health and Allied Sciences	MUHAS	100	Ndani ya nchi	Huduma
26.	Mwalimu Julius K. Nyerere University of Agriculture and Technology	MJNUAT	100	Ndani ya nchi	Huduma
27.	Mwalimu Nyerere Memorial Academy	MNMA	100	Ndani ya nchi	Huduma
28.	Mzumbe University	MU	100	Ndani ya nchi	Huduma
29.	National College of Tourism	NCT	100	Ndani ya nchi	Huduma
30.	National Institute of Transport	NIT	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
31.	National Sugar Institute	NSI	100	Ndani ya nchi	Huduma
32.	Nelson Mandela African Institute of Science and Technology	NM-AIST	100	Ndani ya nchi	Huduma
33.	Open University of Tanzania	OUT	100	Ndani ya nchi	Huduma
34.	Sokoine University of Agriculture	SUA	100	Ndani ya nchi	Huduma
35.	Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo	TASUBA	100	Ndani ya nchi	Huduma
36.	Tanzania Institute of Accountancy	TIA	100	Ndani ya nchi	Huduma
37.	Tanzania Public Service College	TPSC	100	Ndani ya nchi	Huduma
38.	Tengeru Institute of Community Development	TICD	100	Ndani ya nchi	Huduma
39.	University of Dar es Salaam	UDSM	100	Ndani ya nchi	Huduma
40.	University of Dodoma	UDOM	100	Ndani ya nchi	Huduma
41.	Uongozi Institute	UONGOZI	100	Ndani ya nchi	Huduma
42.	Vocational Education and	VETA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Training Authority				
43.	Water Institute	WI	100	Ndani ya nchi	Huduma
44.	Architects and Quantity Surveyors Registration Board	AQRB	100	Ndani ya nchi	Huduma
45.	Contractors Registration Board	CRB	100	Ndani ya nchi	Huduma
46.	Engineers Registration Board	ERB	100	Ndani ya nchi	Huduma
47.	Law School of Tanzania	LST	100	Ndani ya nchi	Huduma
48.	Medical Council of Tanganyika	MCT	100	Ndani ya nchi	Huduma
49.	National Board of Accountants and Auditors	NBAA	100	Ndani ya nchi	Huduma
50.	Pharmacy Council of Tanzania (Pct)	PCT	100	Ndani ya nchi	Ndani ya nchi
51.	Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board	PSPTB	100	Ndani ya nchi	Huduma
52.	Tanzania Nursing and Midwifery Council	TNMC	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
53.	Town Planners Registration Board	TPRB	100	Ndani ya nchi	Huduma
54.	Valuers Registration Board	VRB	100	Ndani ya nchi	Huduma
55.	National Council for Technical and Vocational Education Training	NACTVET	100	Ndani ya nchi	Huduma
56.	National Examinations Council of Tanzania	NECTA	100	Ndani ya nchi	Huduma
57.	Tanzania Commission for Universities	TCU	100	Ndani ya nchi	Huduma
58.	Tanzania Institute of Education	TIE	100	Ndani ya nchi	Huduma
59.	Tanzania Library Service Board	TLSB	100	Ndani ya nchi	Huduma
60.	Unesco National Commission	UNESCO NATCOM	100	Ndani ya nchi	Huduma
61.	Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology	CAMARTEC	100	Ndani ya nchi	Huduma
62.	National Bureau of Statistics	NBS	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
63.	National Institute for Medical Research	NIMR	100	Ndani ya nchi	Huduma
64.	Tanzania Agricultural Research Institute	TARI	100	Ndani ya nchi	Huduma
65.	Tanzania Atomic Energy Commission	TAEC	100	Ndani ya nchi	Huduma
66.	Tanzania Commission for Science and Technology	COSTECH	100	Ndani ya nchi	Huduma
67.	Tanzania Engineering Manufacturing and Design Organization	TEMDO	100	Ndani ya nchi	Huduma
68.	Tanzania Fisheries Research Institute	TAFIRI	100	Ndani ya nchi	Huduma
69.	Tanzania Forest Research Institute	TAFORI	100	Ndani ya nchi	Huduma
70.	Tanzania Industrial Research and Development Organization	TIRDO	100	Ndani ya nchi	Huduma
71.	Tanzania Livestock Research Institute	TALIRI	100	Ndani ya nchi	Huduma
72.	Tanzania Wildlife Research	TAWIRI	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Institute				
73.	Tea Research Institute of Tanzania	TRIT	100	Ndani ya nchi	Huduma
74.	Tobacco Research Institute of Tanzania	TORITA	100	Ndani ya nchi	Huduma
III: Mamlaka za Maji na Mabonde – 43					
1.	Arusha Urban Water Supply and Sanitation Authority	AUWSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Babati Urban Water Supply and Sanitation Authority	BAWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Bariadi Urban Water Supply and Sanitation Authority	BARUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Bukoba Urban Water Supply and Sanitation Authority	BUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Dar Es Salaam Water Supply and Sanitation Authority	DAWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Dodoma Urban Water Supply and Sanitation	DUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Authority				
7.	Geita Urban Water Supply and Sanitation Authority	GEUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
8.	Handeni Trunk Main Water Supply and Sanitation Authority	HTM WSSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
9.	Iringa Urban Water Supply and Sanitation Authority	IRUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
10.	Kahama Shinyanga Water Supply and Sanitation Authority	KASHWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
11.	Kahama Urban Water Supply and Sanitation Authority	KUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
12.	Kigoma Urban Water Supply and Sanitation Authority	KUWASSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
13.	Lindi Urban Water Supply and Sanitation Authority	LUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
14.	Makonde Plateau Water Supply and Sanitation Authority	MAKONDE WSSA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
15.	Masasi-Nachingwea Water Supply and Sanitation Authority	MANAWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
16.	Maswa Water Supply and San- itation Authority	MAUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
17.	Mbeya Urban Water Supply and Sanitation Authority	MBEYA UWSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
18.	Morogoro Water Supply and Sanitation Authority	MORUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
19.	Moshi Urban Water Supply and Sanitation Authority	MUWSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
20.	Mpanda Urban Water Supply and Sanitation Authority	MPUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
21.	Mtwara Urban Water Supply and Sanitation Authority	MTUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
22.	Mugango-Kyabakari Water Supply and Sanitation Authority	MUGANGO WSSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
23.	Musoma Urban Water Supply and Sanitation	MUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Authority				
24.	Mwanza Urban Water Supply and Sanitation Authority	MWAUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
25.	Njombe Urban Water Supply and Sanitation Authority	NJUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
26.	Shinyanga Water Supply and Sanitation Authority	SHUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
27.	Singida Urban Water Supply and Sanitation Authority	SUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
28.	Songea Urban Water Supply and Sanitation Authority	SOUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
29.	Sumbawanga Urban Water Supply and Sanitation Authority	SUWASA RUKWA	100	Ndani ya nchi	Huduma
30.	Tabora Urban Water Supply and Sanitation Authority	TUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
31.	Tanga Water and	TANGA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Sanitation Authority	UWASA			
32.	Vwawa Mlowo Water Supply and Sanitation Authority	VWAWA WSSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
33.	Wanging'ombe Water Supply and Sanitation Authority	WANGIW ASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
34.	Rural Water Supply and Sanitation Agency	RUWASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
35.	Internal Drainage Basin Water Board	IDBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
36.	Lake Nyasa Basin Water Board	LNBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
37.	Lake Rukwa Basin Water Board	LRBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
38.	Lake Tanganyika Basin Water Board	LTBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
39.	Lake Victoria Basin Water Board	LVBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
40.	Pangani Basin Water Board	PBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
41.	Rufiji Basin Water Board	RBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
42.	Ruvuma and Southern Coast Basin Water Board	RSCBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
43.	Wami-Ruvu Basin Water Board	WRBWB	100	Ndani ya nchi	Huduma
IV: Usimamizi na Udhibiti wa Sekta – 22					
1.	Bank of Tanzania	BOT	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Business Registration and Licensing Agency	BRELA	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Capital Markets and Securities Authority	CMSA	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Energy and Water Utilities Regulatory Authority	EWURA	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Fair Competition Commission	FCC	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Gaming Board of Tanzania	GBT	100	Ndani ya nchi	Huduma
7.	Land Transport Regulatory Authority	LATRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
8.	Mining Commission	MC	100	Ndani ya nchi	Huduma
9.	National Environment Management Council	NEMC	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
10.	Petroleum Upstream Regulatory Authority	PURA	100	Ndani ya nchi	Huduma
11.	Public Procurement Regulatory Authority	PPRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
12.	Tanzania Airports Authority	TAA	100	Ndani ya nchi	Huduma
13.	Tanzania Atomic Energy Commission	TAEC	100	Ndani ya nchi	Huduma
14.	Tanzania Bureau of Standards	TBS	100	Ndani ya nchi	Huduma
15.	Tanzania Civil Aviation Authority	TCAA	100	Ndani ya nchi	Huduma
16.	Tanzania Communication Regulatory Authority	TCRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
17.	Tanzania Fertilizer Regulatory Authority	TFRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
18.	Tanzania Insurance Regulatory Authority	TIRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
19.	Tanzania Medicine and Medical Devices Authority	TMDA	100	Ndani ya nchi	Huduma
20.	Tanzania Plant Health and Pesticides Authority	TPHPA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
21.	Tanzania Shipping Agencies Corporation	TASAC	100	Ndani ya nchi	Huduma
22.	Tanzania Trade Development Authority	TANTRADE	100	Ndani ya nchi	Huduma
V: Taasisi za Kilimo – 13					
1.	Agricultural Seed Agency	ASA	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Tanzania Official Seed Certification Institute	TOSCI	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Tanzania Smallholders Tea Development Agency	TSHTDA	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	National Food Reserve Agency	NFRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Cashewnut Board of Tanzania	CBT	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Sugar Board Of Tanzania (Sbt)	SBT	100	Ndani ya nchi	Huduma
7.	Tanzania Coffee Board	TCB COFFEE	100	Ndani ya nchi	Huduma
8.	Tanzania Cotton Board	TCB COTTON	100	Ndani ya nchi	Huduma
9.	Tanzania Fertilizer	TFRA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Regulatory Authority				
10.	Tanzania Pyrethrum Board	TPB	100	Ndani ya nchi	Huduma
11.	Tanzania Sisal Board	TSB	100	Ndani ya nchi	Huduma
12.	Tanzania Tobacco Board	TTB TOBACCO	100	Ndani ya nchi	Huduma
13.	Tea Board of Tanzania	TBT	100	Ndani ya nchi	Huduma
VI: Taasisi za Afya – 6					
1.	Benjamin Mkapa Hospital	BMH	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Jakaya Kikwete Cardiac Institute	JKCI	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Muhimbili National Hospital	MNH	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Muhimbili Orthopaedic Institute	MOI	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Ocean Road Cancer Institute	ORCI	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Tanzania Food and Nutrition Centre	TFNC	100	Ndani ya nchi	Huduma
VII: Mifuko ya Hifadhi za Jamii – 4					
1.	National Health Insurance Fund	NHIF	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
2.	National Social Security Fund	NSSF	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Public Service Social Security Fund	PSSSF	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Workers Compesation Fund	WCF	100	Ndani ya nchi	Huduma
VIII: Uendeshaji wa Sekta – 7					
1.	Agricultural Inputs Trust Fund	AGITF	100	Ndani ya nchi	Huduma
2.	Higher Education Students' Loans Board	HESLB	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	National Water Fund	NWF	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Roads Fund Board	RFB	100	Ndani ya nchi	Huduma
5.	Tanzania Education Authority	TEA	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Tanzania Forest Fund	TAFF	100	Ndani ya nchi	Huduma
7.	Universal Communications Service Access Fund	UCSAF	100	Ndani ya nchi	Huduma
IX : Rufaa za Sheria – 4					
1.	Fair Competition Tribunal	FCT	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
2.	Public Procurement Appeals Authority	PPAA	100	Ndani ya nchi	Huduma
3.	Tax Revenue Appeals Board	TRAB	100	Ndani ya nchi	Huduma
4.	Tax Revenue Appeals Tribunal	TRAT	100	Ndani ya nchi	Huduma
X : Taasisi nyinginezo – 44					
5.	Copyright Society of Tanzania	COSOTA	100	Ndani ya nchi	Huduma
6.	Dar es Salaam Rapid Transport Agency (Dart)	DART	100	Ndani ya nchi	Huduma
7.	Deposit Insurance Board	DIB	100	Ndani ya nchi	Huduma
8.	E-Government Authority	eGA	100	Ndani ya nchi	Huduma
9.	Export Processing Zones Authority	EPZA	100	Ndani ya nchi	Huduma
10.	Geological Survey Of Tanzania	GST	100	Ndani ya nchi	Huduma
11.	Government Chemist Laboratory Authority	GCLA	100	Ndani ya nchi	Huduma
12.	Government Procurement Services Agency	GPSA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
13.	Marine Parks And Reserves Unit	MPRU	100	Ndani ya nchi	Huduma
14.	National Arts Council	BASATA	100	Ndani ya nchi	Huduma
15.	National Construction Council	NCC	100	Ndani ya nchi	Huduma
16.	National Economic Empowerment Council	NEEC	100	Ndani ya nchi	Huduma
17.	National Identification Authority	NIDA	100	Ndani ya nchi	Huduma
18.	National Kiswahili Council	BAKITA	100	Ndani ya nchi	Huduma
19.	National Land Use Planning Commission	NLUPC	100	Ndani ya nchi	Huduma
20.	National Museum of Tanzania	NMT	100	Ndani ya nchi	Huduma
21.	National Sports Council of Tanzania	NSCT	100	Ndani ya nchi	Huduma
22.	Occupational Safety and Health Authority	OSHA	100	Ndani ya nchi	Huduma
23.	Petroleum Bulk Procurement Agency	PBPA	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
24.	Registration Insolvency and Trusteeship Agency	RITA	100	Ndani ya nchi	Huduma
25.	Rural Energy Agency	REA	100	Ndani ya nchi	Huduma
26.	Small Industries Development Organization	SIDO	100	Ndani ya nchi	Huduma
27.	Tanzania Buildings Agency	TBA	100	Ndani ya nchi	Huduma
28.	Tanzania Electrical, Mechanical and Electronics Services Agency	TEMESA	100	Ndani ya nchi	Huduma
29.	Tanzania Extractive Industries Transparency Initiative	TEITI	100	Ndani ya nchi	Huduma
30.	Tanzania Film Board	TFB	100	Ndani ya nchi	Huduma
31.	Tanzania Fisheries Corporation	TAFICO	100	Ndani ya nchi	Huduma
32.	Tanzania Forest Service Agency	TFS	100	Ndani ya nchi	Huduma
33.	Tanzania Government Flights Agency	TGFA	100	Ndani ya nchi	Huduma
34.	Tanzania Investment Centre	TIC	100	Ndani ya nchi	Huduma

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
35.	Tanzania Meteorological Authority	TMA	100	Ndani ya nchi	Huduma
36.	Tanzania National Business Council	TNBC	100	Ndani ya nchi	Huduma
37.	Tanzania National Roads Agency	TANROADS	100	Ndani ya nchi	Huduma
38.	Tanzania Revenue Authority	TRA	100	Ndani ya nchi	Huduma
39.	Tanzania Rural and Urban Road Agency	TARURA	100	Ndani ya nchi	Huduma
40.	Tanzania Tourist Board	TTB TOURIST	100	Ndani ya nchi	Huduma
41.	Tanzania Veterinary Laboratory Agency	TVLA	100	Ndani ya nchi	Huduma
42.	Tanzania Wildlife Management Authority	TAWA	100	Ndani ya nchi	Huduma
43.	Warehouse Receipts Regula- tory Board	WRRB	100	Ndani ya nchi	Huduma
44.	Weights and Measures Agency	WMA	100	Ndani ya nchi	Huduma

2.0 KIAMBATISHO 02: ORODHA YA UWEKEZAJI WA SERIKALI KWENYE TAASISI AMBAPO SERIKALI INA *HISA CHACHE (MIS)*

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
I: Kampuni za Mawasiliano - 2					
1.	Airtel Tanzania Plc.	AIRTEL	49	Ndani ya nchi	Biashara
2.	DATEL Tanzania Limited (A-Link Telecom Tanzania Limited)	DATEL	35	Ndani ya nchi	Biashara
II: Kampuni za Ujenzi – 1					
3.	Mwananchi Engineering and Construction Company Limited	MECCO	25	Ndani ya nchi	Biashara
III: Kampuni za Nishati- 3					
4.	PUMA Energy Tanzania Limited	PUMA	50	Ndani ya nchi	Biashara
5.	Tanzania Zambia Mafuta Pipeline Limited	TAZAMA	50	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
6.	Tanzania International Petroleum Reserves Limited	TIPER	50	Ndani ya nchi	Biashara
III: Kampuni za Madini- 6					
7.	Bulyanhulu Gold Mine Limited	BGML	16	Ndani ya nchi	Biashara
8.	Mbeya Cement Company Limited	MCCL	25	Ndani ya nchi	Biashara
9.	North Mara Gold Mine Limited	NMGML	16	Ndani ya nchi	Biashara
10.	TEMBO Nickel	TEMBO	16	Ndani ya nchi	Biashara
11.	TWIGA Minerals Company Limited	TWIGA	16	Ndani ya nchi	Biashara
12.	Williamson Diamond Limited	WDL	37	Ndani ya nchi	Biashara
III: Kampuni za Huduma za Kifedha – 16					
13.	Dar es Salaam Stock Exchange	DSE	15	Ndani ya nchi	Biashara
14.	Industrial Promotion	IPS	18.2	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Services (T) Limited				
15.	NBC Limited	NBC	30	Ndani ya nchi	Biashara
16.	NMB Bank Plc.	NMB	31.8	Ndani ya nchi	Biashara
17.	Tanzania Re-Insurance Company Limited	TAN RE	Golden Share	Ndani ya nchi	Biashara
18.	Tanzania Development Finance Limited	TDFL	32	Ndani ya nchi	Biashara
19.	African Development Bank	AfDB	0.76	Nje ya nchi	Biashara
20.	African Re-Insurance Corporation	AFRICA RE 0	0.8	Nje ya nchi	Biashara
21.	African Trade Insurance Agency	ATIA	8.37	Nje ya nchi	Biashara
22.	East Africa Development Bank	EADB	26.32	Nje ya Nchi	Biashara
23.	East and Southern Africa Trade and Development Bank	TDB	8.33	Nje ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
24.	International Development Association	IDA	0.24	Nje ya nchi	Biashara
25.	International Finance Corporation	IFC	0.07	Nje ya nchi	Biashara
26.	Multilateral Investment Guarantee Agency	MIGA	0.22	Nje ya nchi	Biashara
27.	Shelter Afrique	S. AFRIQUE	0.7	Nje ya nchi	Biashara
28.	World Bank (International Bank for Reconstruction Development)	IBRD	0.06	Nje ya nchi	Biashara
IV: Kampuni za Uzalishaji - 16					
29.	ALAF Limited	ALAF	24	Ndani ya nchi	Biashara
30.	Abood Seed Oil Limited	ASOIL	20	Ndani ya nchi	Biashara
31.	East African Cables (T) Limited	EA CABLES	29	Ndani ya nchi	Biashara
32.	Friendship Textile	FTC	50	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
	Company Limited	(URAFIKI)			
33.	Keko Pharmaceuticals (1997) Limited	KPIL	40	Ndani ya nchi	Biashara
34.	Kilombero Sugar Company Limited	KSCL	25	Ndani ya nchi	Biashara
35.	Mbinga Coffee Curing Company Limited	MBINGA CCC	43	Ndani ya nchi	Biashara
36.	Mbozi Coffee Curing Company Limited	MBOZI CCC	32	Ndani ya nchi	Biashara
37.	Moshi Leather Industries	MLI	25	Ndani ya nchi	Biashara
38.	TANELEC Limited	TANELEC	30	Ndani ya nchi	Biashara
39.	Tanganyika Instant Coffee	TANICA	7.7	Ndani ya nchi	Biashara
40.	Tanzania Cigarette Company Limited	TCC	2.2	Ndani ya nchi	Biashara
41.	TLL Printing and Packaging Limited	TLLPPL	9	Ndani ya nchi	Biashara
42.	TOL Gases Limited	TOL 6	6.2	Ndani ya nchi	Biashara
43.	TPC Limited	TPC	25	Ndani ya nchi	Biashara

Na.	Jina	Kifupi	% ya Umiliki	Eneo la Uendeshaji	Asili ya Uendeshaji
44.	Tanzania Pharmaceuticals Industries	TPI	40	Ndani ya nchi	Biashara
V: Kampuni za Uchakataji - 1					
45.	TANSCAN Timber Limited	TANSCAN	49	Ndani ya Nchi	Biashara
VI: Kampuni za Usafirishaji – 3					
46.	Chinese Tanzania Joint Shipping Company Limited	SINOTASHIP	50	Ndani ya Nchi	Biashara
47.	Tanzania Zambia Railways Authority	TAZARA	50	Ndani ya nchi	Biashara
48.	UDA Limited	UDA	49	Ndani ya nchi	Biashara
VI: Kampuni za Huduma za Kitalii					
49.	Inflight Catering Services Limited	ICSL	29	Ndani ya nchi	Biashara
50.	New Africa Hotel	NAH	23	Ndani ya nchi	Biashara